# STANDARD 5 KISWAHILI
# MID-TERM 1 2020

*MUDA: Saa1 dakika 40*

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.*

Tabia __1__ ni kitu __2__ kila mwanafunzi __3__ kuwa macho. Mwanafunzi __4__ tabia njema huheshimiwa na __5__ na kila mtu. Lakini mwanafunzi fidhuli na __6__ hudharauliwa na __7__ na wenzake. Yeye hubaki pweke __8__ rafiki.

Sisi __9__ wanafunzi yatupasa tuwe na heshima kwa __10__, wazazi, walimu na watu __11__ katika jamii, chambilecho wahenga heshima si __12__.

Tabia njema na bidii __13__ ufunguo wa ufanisi, __14__ kila mwanafunzi anapaswa __15__ nao.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. zuri | B. kizuri | C. nzuri | D. mzuri |
| 2. | A. ambayo | B. ambacho | C. ambaye | D. ambalo |
| 3. | A. hafai | B. anaweza | C. hawezi | D. anafaa |
| 4. | A. mwenye | B. yenye | C. chenye | D. wenye |
| 5. | A. kupenda | B. kupendana | C. kupendewa | D. kupendwa |
| 6. | A. mcheshi | B. mchokozi | C. mchezaji | D. mpole |
| 7. | A. kutorokwa | B. kutorokewa | C. kukimbiliwa | D. kuhepwa |
| 8. | A. na | B. pamoja na | C. bila | D. hata na |
| 9. | A. mbona | B. kama | C. nao | D. nanyi |
| 10. | A. wezetu | B. wenjetu | C. wenzietu | D. wenzetu |
| 11. | A. kote | B. sote | C. wote | D. nyote |
| 12. | A. ujinga | B. upumbavu | C. utumwa | D. upweke |
| 13. | A. ndio | B. ndiyo | C. ndiwo | D. ndizo |
| 14. | A. ambako | B. ambazo | C. ambalo | D. ambao |
| 15. | A. kua | B. kuwa | C. kukua | D. kukuwa |

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16. Andika sentensi hii katika hali ya wingi**

*Mbuzi wangu amechinjwa*

A. Mbuzi zetu zimechinjwa.
B. Mbuzi wangu wamechinjwa.
C. Mbuzi wetu amechinjwa.
D. Mbuzi wetu wamechinjwa.

**17. Kanusha sentensi ifuatayo**

*Baba anakuja*

A. Baba anaenda. B. Baba hakujangi.
C. Baba haji. D. Baba haendi.

**18.** Neno 'sanduku' liko katika ngeli gani?

A. I - ZI B. LI - YA
C. I - I D. U - ZI

**19.** Ni sentensi gani imetumia -ote- kwa usahihi

A. Sisi wote tutasafiri.
B. Maji zote zimemwagika.
C. Magari zote zimeharibika.
D. Vyoo vyote vimebomoka.

**20. Tumia -o-ote kwa usahihi**

*Nitaendesha gari* ______

A. lolote. B. yoyote.
C. chochote. D. wowote.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

21. **Kamilisha kwa kivumishi sahihi**
*Nitatumia nyundo _______ kuvunja mlango huu.*
A. lolote B. yoyote
C. chochote D. wowote

22. Ni sentensi gani imetumia kiulizi **-ipi-** kwa usahihi?
A. Ni gari ipi imeibwa?
B. Ni chupa kipi kimevunjika?
C. Ni chai ipi imenywewa?
D. Ni shati ipi imefuliwa?


23. Ni sentensi ipi imetumia **'yenyewe'** kwa usahihi?
A. Ugali yenyewe imeiva.
B. Ukuta umebomoka yenyewe.
C. Choo yenyewe ni nzuri.
D. Maua yenyewe yanapendeza.

24. Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita
*Baba anasoma gazeti*
A. Baba atasoma gazeti.
B. Baba alisoma gazeti.
C. Baba amesoma gazeti.
D. Baba husoma gazeti.

25. **Kamilisha sentensi ifuatayo**
*Walienda Mombasa _______*
A. na gari.
B. pamoja na gari.
C. kwa gari.
D. kwenye gari.

26. Maelezo sahihi ya shangazi ni _______
A. Ndugu wa kike wa mama.
B. Ndugu wa kiume wa baba.
C. Ndugu wa kike wa baba.
D. Ndugu wa kiume wa mama.

27. Umbo hili huitwa _______



A. duara dufu. B. duara.
C. tufe. D. mviringo.

28. **Kamilisha methali ifuatayo**
*Mwenye macho _______*
A. huona. B. haambiwi tazama.
C. si kipofu. D. huangaza.

29. Chagua istiara kati ya hizi
A. Mtu huyu ni sungura.
B. Amekonda kama ng'onda.
C. Bingiria bingiribingiri.
D. Bandubandu huisha gogo.

30. Tegua kitendawili hiki.
Nyumba yangu ina nguzo moja
A. yai. B. mwavuli.
C. uyoga. D. mti.

*<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.</u>*

Elimu ni kitu cha maana sana katika maisha ya binadamu. Elimu imefananishwa na nuru; nuru ambayo ikimwangazia mtu humtoa katika giza. Hebu fikiria maisha bila nuru yangekuaje? Ingekuwa vigumu mtu kutembea kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine. Na iwapo mtu angejaribu kutembea, basi angekumbana na masaibu makubwa kama vile kutumbukia kwenye mashimo marefu, kugongana na miti au hata kushambuliwa na wanyama wakali. Angekabiliwa na njaa kwa kukosa chakula. Maisha yangekuwa magumu na mafupi.

Mtu anapopata elimu, na si elimu tu, bali elimu bora, ni sawa na mtu aliyeangaziwa nuru. Elimu humwezesha mtu kukabiliana na changamoto zote za maisha. Mfano wa changamoto hizo ni ujinga, maradhi na umaskini. Hawa ndio maadui wetu wakubwa kama watu binafsi na kama taifa.

Taifa letu la Kenya limepiga hatua kubwa kimaendeleo kutokana na elimu ya watu wake. Baada ya kupata uhuru rais wa kwanza Mzee Jomo Kenyatta alitangaza vita dhidi ya maadui watatu: Ujinga (kukosa elimu), maradhi na umaskini. Marais wote waliofuata pia ***<u>walishikilia uzi huohuo</u>***. Na vita hivyo bado vinaendelea hadi sasa. Tuache vita vya kikabila.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Katika bara la Afrika Kenya imepiga hatua kubwa sana ukilinganisha na nchi nyingine. Elimu hii ndogo îmetuwezesha kupigana na umaskini na kuinua uchumi wa nchi. Wakati huo huo pia tumeweza kupambana na maradhi kupitia kuwaelimisha wananchi kuhusu kanuni za afya.

Tuache vita vya kikabila na tuungane katika vita dhidi ya maadui hawa watatu wa taifa letu.

---

**31.** Elimu imefananishwa na nini katika kifungu hiki?
A. Kitu cha maana.
B. Taa.
C. Mwangaza.
D. Mwenge.

**32.** Ni masaibu gani amabayo hayakutajwa?
A. Kuumwa na nyoka.
B. Kutumbukia kwenye mashimo.
C. Kugongana na miti.
D. Kushambuliwa na wanyama.

**33.** Neno ***'ujinga'*** kama changamoto limetumiwa kumaanisha
A. ukosefu wa ajira.
B. upungufu wa akili.
C. ukosefu wa elimu.
D. ukosefu wa amani.

**34.** Ni nini kimesaidia taifa letu kupiga hatua kimaendeleo?
A. Kilimo. B. Elimu.
C. Madini. D. Utalii.

**35.** Ni rais gani aliyetangaza vita dhidi ya maadui wetu watatu?
A. Moi. B. Uhuru.
C. Jomo. D. Kibaki.

**36.** Maneno kushikilia uzi huo huo yamepigwa mstari. Yana maanisha
A. kushikilia uzi usikatike.
B. kupiga vita wakoloni.
C. kupiga vita ufisadi.
D. kuendeleza vita dhidi ya maadui wetu watatu.

**37.** Ni vita gani visivyofaa kupiganwa?
A. Vita dhidi ya ufisadi.
B. Vita vya kikabila.
C. Vita dhidi ya mihadarati.
D. Vita dhidi ya umaskini.

**38.** Ni neno gani haliwezi kutumika badala ya elimu?
A. Masomo. B. Ujuzi.
C. Upuzi. D. Maarifa.

**39.** Elimu inayoweza kuleta maendeleo ni
A. Elimu bora.
B. Elimu ya kawaida.
C. Elimu duni.
D. Elimu ya wastani.

**40.** Kichwa kifaacho taarifa hii ni
A. maendeleo ya nchi yetu.
B. maadui wetu watatu.
C. nuru ya maisha.
D. umuhimu wa elimu.

---

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Hapo zamani paliondokea vijana wawili marafiki sana. Mmoja aliitwa Janja na mwingine Janjaure. Marafiki hawa walipendana sana kama chanda na pete. Alipokuwepo Janja alikuwepo Janjaure na alipokuwepo Janjaure alikuwepo Janja. Vijana hawa waliishi mtaa mmoja na pia walisoma shule moja na katika darasa moja.

Janjaure alikuwa na tabia ya kwenda shuleni bila vitabu. Alikuwa akibeba kalamu, karatasi moja na kitabu cha hadithi. Huko darasani alikuwa akisumbua wanafunzi wenzake kwa kelele. Waliojaribu kusoma aliwatatiza na kuwapotosha kwa kuwashauri kuwa hakuna haja ya kusoma sana kwa kuwa akili nyingi huondoa maarifa. Lile ambalo hakuwafichulia wanafunzi wenzake ni kuwa kule nyumbani yeye alikuwa akisoma kama mwendawazimu wa vitabu. Shuleni alijitia kusoma kitabu cha hadithi darasani hata mwalimu akifundisha. Kumbe alikuwa ni ujanja tu. Masikio yake yalikuwa kama ya sungura akiyashika yote mwalimu aliyokuwa akifundisha na kunakili mada kwenye karatasi. Alipofika nyumbani alidurusu ***barabara***.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Maskini rafiki yake Janja alimwamini kuwa hakuwa akisoma. Kwa kuwa ni rafiki yake aliamua kuiga mtindo wake. Alianza kubeba kitabu cha hadithi na kusoma wakati mwalimu anafundisha. Alijiunga na rafiki yake Janjaure kuwatatiza wanafunzi wenzake wanaposoma.

Wakati wa mtihani wa mwisho wa darasa la nane ulifika. Walifanya mtihani na kungoja matokeo. Matokeo yalipotokea Janjaure ndiye aliyekuwa akiongoza wenzake wote katika madarasa matatu ya nane; na Janja ndiye aliyekuwa akishikilia mkia. Wanafunzi walimshangaa sana Janjaure na kudhani kuwa ulikuwa uchawi au wizi wa mtihani. Lakini walimsikitikia Janja kwa kupoteza wakati wake na rafiki mjanja.

---

**41.** Janja na Njanjaure walipendana kama chanda na pete au pia twaweza kusema
A. uta na upote.
B. uzi na sindano.
C. jembe na mpini.
D. kiatu na soksi.

**42.** Janja na Janjaure walikuwa na tabia gani darasani?
A. Wasikivu na wazingativu.
B. Makini na wa kuwajibika.
C. Wasumbufu na wazembe.
D. Watiifu na wenye bidii.

**43.** Kati ya Janja na Janjaure ni nani aliyekuwa mwerevu?
A. Janja.
B. Janjaure.
C. Wote.
D. Hakuna.

**44.** Ni jambo gani ambalo wanafunzi hawakujua kuhusu Janjaure?
A. Alikuwa msumbufu.
B. Alikuwa mzembe.
C. Alikuwa rafiki ya Janja.
D. Alikuwa akisomea nyumbani.

**45.** Twaweza kusema kuwa urafiki wa Janja na Janjaure
A. ulikuwa wa dhati.
B. haukuwa wa kweli.
C. ulikuwa wa maana.
D. ulikuwa wa faida.

**46.** Maneno *"Akili nyingi huondoa maarifa"* ni
A. methali.
B. kitendawili.
C. tashbihi.
D. istiara.

**47.** Neno *'barabara'* limepigwa mstari, linamaanisha
A. njia kuu
B. ovyovyo.
C. juu juu.
D. kwa makini.

**48.** Ni methali gani inayoeleza tabia ya Janja?
A. Jungu kuu halikosi ukoko.
B. Mtoto akililia wembe mpe.
C. Bendera hufuata upepo.
D. Baniani mbaya kiatu chake dawa.

**49.** Ni funzo gani tunalopata katika hadithi hii
A. hata usiposoma waweza kufaulu.
B. si lazima tubebe vitatu shuleni.
C. usiamini sana kila mtu, hata rafiki.
D. akili si kusoma sana.

**50.** Kichwa kinachofaa hadithi hii ni
A. Urafiki wa maana.
B. Urafiki wa bandia.
C. Marafiki waaminifu.
D. Urafiki wa kweli.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com